Idara ya Kazi ya Marekani

OSHA®
Utawala wa Usalama na Afya Kazini

# Usalama na Afya Kazini
# HII NI SHERIA!

### Wafanyakazi wote wanayo haki ya:

- Kuwa na mahali salama pa kazi.
- Kutoa maoni kuhusu usalama au afya kwa mwajiri wako au OSHA, au kuripoti jeraha au ugonjwa uliotokana na kazi, bila kulipizwa kisasi.
- Kupokea taarifa na mafunzo kuhusu hatari za kazini, ikiwa ni pamoja na vitu vyote hatari kwenye eneo lako la kazi.
- Kuomba ukaguzi wa siri wa OSHA wa mahali pako pa kazi endapo unaamini kuwa kuna hali zisizo salama au ni mbaya. Una haki ya kuwa na mwakilishi wa kuwasiliana na OSHA kwa niaba yako.
- Kushiriki (au mwakilishi wako kushiriki) kwenye ukaguzi wa OSHA na uzungumze kwa faragha na mkaguzi.
- Kutuma malalamiko kwa OSHA ndani ya siku 30 (kwa simu, mtandaoni au barua) endapo umelipizwa kisasi kwa kudai haki zako.
- Kutazama dondoo zozote za OSHA zinazotolewa kwa mwajiri wako.
- Kuomba nakala za rekodi zako za matibabu, vipimo vinavyopima hatari za mahali pa kazi, na kumbukumbu ya majeraha na magonjwa mahali pa kazi.

### Waajiri wanapaswa:

- Kuwezesha hali ya usalama kwa wafanyakazi mahali pa kazi na bila ya uwepo wa hatari zinazojulikana. Ni kinyume cha sheria kulipiza kisasi dhidi ya mfanyakazi kwa kutumia haki zake zozote chini ya sheria, ikiwa ni pamoja na kuzungumzia suala la afya na usalama kwako au kwa OSHA, au kuripoti kuhusu jeraha au ugonjwa uliotokana na kazi.
- Kuzingatia viwango vyote vinavyotumika vya OSHA.
- Kuitaarifu OSHA ndani ya masaa 8 baada ya kifo kilichotokea mahali pa kazi au ndani ya masaa 24 baada ya kulazwa hospitalini kwa wagonjwa, kukatwa kiungo au kupoteza jicho mahali pa kazi.
- Kutoa mafunzo yanayohitajika kwa wafanyakazi wote kwa kutumia lugha na msamiati wanaoweza kuuelewa.
- Kuonesha bango hili kwa uwazi mahali pa kazi.
- Kuchapisha dondoo za OSHA mahali au karibu na eneo la madai ya ukiukaji wa haya masuala.

Huduma za Ushauri Kazini zinapatikana kwa waajiri wadogo na wa kati, bila shida au adhabu, kupitia mipango ya mashauriano inayoungwa mkono na OSHA katika kila jimbo.

*Bango hili linapatikana bila malipo kutoka OSHA.*

***Wasiliana na OSHA. Tunaweza kusaidia.***



**1-800-321-OSHA (6742) • TTY 1-877-889-5627 • www.osha.gov**

SHA 4406-03 2024
s the Law – Swahili

Source: OSHA (osha.gov) | Traduit par https://hseacademy.online/